# MWANASHERIA

JARIDA LA AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

AGC ZANZIBAR ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

TOLEO LA 001 JANUARI - JUNI 2024




# "HAKI NA WAJIBU"

SCAN ME

Scan kusoma Jarida kielektroniki

WWW.AGCZ.GO.TZ

**HALIUZWI**

# SALAMU ZA MWANASHERIA MKUUU



**Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, mara kwa mara imekuwa inasisitiza umuhimu wa taasisi za umma kutoa taarifa kuhusiana na shughuli zinazotekelezwa na taasisi hizo, ili kueleza matokeo ya utekelezaji wake.**

Taasisi hizo hutumia njia tofauti kutekeleza maagizo hayo, ikiwemo njia ya kuchapisha na kusambaza majarida. Miongoni mwa malengo ya majarida hayo ni kutoa elimu kwa umma ili kuwapatia uelewa watu mbali mbali wakiwemo wadau wa huduma au bidhaa zinazotolewa na taasisi hizo.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, nayo imeanzisha jarida ili kutekeleza wito wa Serikali wa kutoa taarifa na elimu kwa umma.

Jarida hili ambalo linajulikana kwa jina la "Mwanasheria" litahusika na utoaji wa elimu kuhusiana na masuala ya kisheria kwa ujumla.

Lakini mkazo utawekwa juu ya mambo yanayohusika na utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Afisi yetu. Aidha, Jarida hili linatarajiwa kutoka kila baada ya miezi sita kwa kuanzia, sawa na na matoleo mawili kwa mwaka.

Majukumu hayo yanabainishwa na Katiba ya Zanzibar ya 1984 katika kifungu cha 56 na Sheria ya Kuanzishwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nam. 6 ya 2013 katika kifungu cha 14(1) – (4).

Majukumu hayo ni kutoa ushauri wa kisheria na kutekeleza shughuli nyengine za kisheria za SMZ, usimamizi wa kesi za madai zinazoishusu Serikali, Uandishi wa miswada ya sheria, kanuni na hati za kisheria na utoaji wa huduma na ushauri wa mikataba.

Pamoja na majukumu hayo, jarida pia litahusika na utoaji wa mada kuhusu masuala mtambuka ya nchi na ya kimataifa yakiwemo Haki za Binadamu, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya rushwa. Maeneo mengine ni mapambano dhidi ya udhalilishaji, masuala ya maadili katika utumishi na mengineyo.

Nachukua fursa hii kuwakaribisha viongozi wa Serikali, watendaji wa taasisi za umma na taasisi za binafsi pamoja na wananchi kwa jumla watakaopata fursa ya kupata nakala za jarida letu, kulisoma kwa ajili ya kujiongezea maarifa na upeo wa kuelewa masuala yanayohusu sheria pamoja na mambo mengine yatakayoandikwa kuhusu mada, matukio na taarifa na mbali mbali.

Baada ya maelezo hayo, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kukamilisha Toleo hili.

Pili, tuna wajibu kuwashukuru watendaji na watumishi wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu walioshiriki katika kufanikisha maandalizi ya Toleo, hasa hasa Bodi ya Wahariri ambayo inaongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu.

Vile vile, tunawashukuru wachangiaji wa Jarida hili walioandaa mada ambazo zimepata nafasi katika toleo hili. Aidha, tunatanguliza shukrani kwa watu wote watakaopata nafasi ya kusoma Toleo hili, kwa kutumia muda wao vyema. Tunatumai baada ya kusoma jarida letu watakuwa wachangiaji wa wazuri wa Jarida letu na kutoa maoni, ambayo tutayathamini na kuyatumia kwa kuliimarisha.

**Dkt. Mwinyi Talib Haji,**
**Mwanasheria Mkuu,**
**Zanzibar.**

AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

**Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar**
**S.L.P 259**
**Mazizini, Zanzibar, Tanzania.**
**Simu : + 255 22 233455**
**barua pepe: agcsmz@agcz.go.tz**
**www.agcz.go.tz**

SCAN ME




**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti**
Shaaban Ramadhan Abdalla
(Naibu Mwanasheria Mkuu)

**Wajumbe**
Mdungi M. Mdungi,
Salim M. Abdalla
Asya M. Ahmed
Shufaa A. Khamis
Abeid M. Saleh
Hamisa M. Mmanga,
Faki H. Mjaka,

**Msanifu**
Abdulghani I. Zubeir

**Mshauri**
Ramadhan M. Suleiman


# TAHARIRI

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kutoa Toleo hili la kwanza la Jarida la "Mwanasheria". Hii ilikuwa ni ndoto ya uongozi wa Afisi yetu ambayo sasa imekuwa kweli. Sina budi kukiri kwamba imechukua muda mrefu kwa Afisi yetu mpaka kufikia hatua hii. Hakika hili ni jambo jema sana!

Toleo hili la "Mwanasheria", lina makala mbili (2). Makala hizo ni Historia Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Mchakato wa Kutunga Sheria Zanzibar. Lengo la msingi la Toleo hili la kwanza ni kuitambulisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia mada ya Historia ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kueleza baadhi ya shughuli ambazo Afisi ya Mwanasheria Mkuu inazifanya. Katika Toleo hili shughuli hizo zinaelezwa katika mada mbili.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu ndio inayohusika na uandishi wa Miswada ya Sheria, hasa Miswada ya Serikali. Vile vile, Afisi hii ndio inayofungua kesi au kuwasilisha madai Mahakamani kwa niaba ya Serikali, inapotokea haja ya Serikali kushtaki, Kushtakiwa au kuwasilisha madai Mahakamani. Kwa kuweka mada hizi katika Toleo hili, tunalenga wasomaji wetu wapate uelewa ingawa kwa uchache, kuhusu Afisi ya Mwanasheria Mkuu inavyotekeleza majukumu yake katika maeneo hayo. Pamoja na mada hizo, Toleo hili linazungumzia mada moja muhimu kwa mazingira ya nchi yetu ambayo ni kuhusu utungaji wa Sheria. Kwa Wazanzibari wengi mada hizi ni muhimu kwa sababu zinagusa maisha ya watu kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Katika kuyafikia mafanikio haya hatuwezi kusahau kazi kubwa iliyofanywa na wahusika mbali mbali. Kwanza kabisa, kwa niaba ya Bodi ya Wahariri ya Jarida hili, ninatoa shukrani za dhati kabisa kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa usimamizi wake. Pili, tunawashukru wataalamu wote waliochangia mada pamoja na taarifa mbali mbali zilizopata nafasi katika Toleo hili, kwa moyo wao wa kujitolea katika kufanikisha kazi hii.

Vilevile, shukrani hizi tunapenda ziwafikie watumishi wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu waliohusika katika maandalizi ya kazi hii kwa njia moja au nyengine. Pamoja na hao, Toleo hili limekamilika kwa kazi kubwa ya Wajumbe wa Bodi ya Wahariri, kwa kazi yao nzuri na busara zao katika upembuzi na uthibitishaji wa mada za Toleo hili.

Mwisho kabisa, tunawatakia wasomaji wetu watarajiwa usomaji mwema wa Jarida letu. Kwa moyo mkunjufu tunawaarifu kuwa tuko tayari kupokea mawazo na maoni yao kwa ajili ya kuliimarisha na kulikuza Jarida letu. Tunapokea Mawazo na maoni hayo kwa kutumia anuani za mawasiliano zifuatayo:


**Afisi ya Mwanasheria Mkuu**
**Zanzibar**
**S.L.P 259**
**Mazizini, Zanzibar, Tanzania.**
**Simu : + 255 22 233455**
**barua pepe: agcsmz@agcz.go.tz**
**www.agcz.go.tz**


**Shaaban Ramadhan Abdalla**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wahariri**

# Mhe. Haroun atahadharisha ufungaji mikataba bila ushauri wa Mwanasheria Mkuu



*Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman akizungumza na Wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu (hawapo pichani) wakati alipotembelea Afisi hiyo, kushoto ni Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji.*

**Na Mwandishi wetu**

***TAASISI za Serikali nchini zimetakiwa kuacha tabia ya kuingia katika Hati za Makubaliano (MOU) na Mikataba mbali mbali bila kupata ushauri wa kisheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar.***

Wito huo umetolewa na Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman wakati alipotembelea Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa lengo la kusikiliza taarifa za utekelezaji.

Waziri huyo alisema ni makosa kwa Taasisi yoyote ya Serikali kuingia mkataba bila kuishirikisha Afisi hiyo kwa kudhani kuwa hakuna ulazima wa kufanya hivyo jambo ambalo ni hatari kwa maendeleo ya taasisi husika na Serikali kwa ujumla

Mhe. Horoun alisema zipo baadhi ya Taasisi hujiamini na kuingia mikataba bila kuishirikisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambapo baadae hukutwa na tatizo ikiwemo kushitakiwa hukimbilia Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupata msaada.

"Ukweli ni kwamba zipo baadhi ya taasisi hujiona wao wanajua zaidi, wana-tayarisha mambo yao huko, wakikwama wanaelekea kwa Mwanasheria Mkuu, hivi sivyo. Ni dhambi kubwa na hatari kwa Taasisi na Serikali kwa ujumla kuingia mkataba bila ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa na taarifa", alisisitiza Mhe. Haroun.

Katika kuondoa changamoto hiyo, Waziri Haroun, aliitaka Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuitisha kikao na Makatibu wakuu wa Wizara na Wakuu wa Taasisi ili kuwapa elimu kuhusu muelekeo wa Serikali ya awamu ya nane juu ya suala la kufunga mikataba.

Alibainisha kuwa inawezekana wapo baadhi ya viongozi wana uelewa mdogo na matokeo yao huingia katika makosa bila kudhamiria kwa sababu tu ya kukosa ufahamu, hivyo watakapofahamishwa changamoto hiyo inaweza kuondoka.

Waziri Haroun alitumia nafasi hiyo kuipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mafanikio makubwa iliyoyapata katika uendeshaji huku akiusisitiza uongozi kuwajengea uwezo wafanyakazi wake.

"Awamu hii mambo ni mengi, naomba uongozi uongeze kasi ya kutoa fursa za masomo kwa wafanyakazi wote, mwenye stashahada akachukue shahada

ya kwanza, mwenye shahada ya kwanza afanye ya pili na kuendelea ili Serikali iwe na watu mahiri wa kuitetea", alisema Waziri huyo.

Awali akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa kipindi cha 2020 hadi Julai 2023 Mwanasheria Mkuu Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji, alisema shughuli za usimamizi wa kesi, mikataba na uandishi wa sheria zimefanyika kwa ufanisi mkubwa.

Alisema katika kipindi hicho jumla ya kesi 139 zilisikilizwa mahkamani ambapo kesi 17 kati ya hizo zilifunguliwa katika kipindi hicho.

Aidha jumla ya kesi 15 zilimalizika na Serikali ilishinda jumla ya kesi 13 na kushindwa katika kesi mbili.

Dkt. Mwinyi alisema Afisi imechukua hatua na kukata Rufaa katika kesi moja na kwa upande wa kesi nyengine iliyosalia, upande wa pili wa wadaiwa wameshawasilisha notisi ya kukata rufaa katika Mahkama ya Rufaa Tanzania.

Dkt. Mwinyi alifahamisha kuwa, katika kipindi hicho, jumla ya indhari 32 za kuishitaki Serikali zimepokelewa na kufuatiliwa katika taasisi husika.

Kwa upande wa Uandishi wa Sheria Mwanasheria Mkuu, alisema, kwa kushirikiana na Taasisi husika, jumla ya Miswada 24 na Kanuni 101 imeandaliwa, huku matangazo mengine ya kisheria 446 yaliandaliwa na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kuhusu usimamizi wa mikataba alisema sekta ya mikataba imeimarika ambapo jumla ya mikataba 2,087 imetolewa ushauri wa kitaalam, kati ya mikataba hiyo 1,330 inahusu ununuzi wa bidhaa na huduma. Mikataba 371 inahusu ujenzi, 223 ni ushauri elekezi, 163 inahusu Kodi.

Aidha, jumla ya hati za makubaliano (MoU) 345 zimetolewa ushauri katika sekta ya elimu, uchumi, usafiri, utalii, makaazi, afya, ardhi, ujenzi, teknolojia, kilimo, utamaduni, sheria, mazingira na fedha.

Akizungumzia changamoto Mwanasheria Mkuu, alisema miongoni mwa changamoto zinazoikabili Afisi hiyo ni pamoja na ufinyu wa Jengo kutokana na ongezeko la Wafanyakazi.

Alifahamisha kuwa jengo la Afisi hiyo haliwezi kuongezwa urefu kulingana na namna lilivyojengwa hivyo alimuomba Mhe. Waziri Haroun kusaidiana ili ku-patikana kwa eneo litakalokidhi mahitaji ya Afisi.

Kadhaalika aliigusia changamoto ya usafiri akisema kuwa Afisi ina uhaba wa gari jambo linalozorotesha utendaji wa majukumu yao hasa katika ufuatiliaji wa kesi.





***Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji akizungumza na Wafanyakazi wa Afisi yake kuhusu utekelezaji wa majukumu yao.***

# Ifahamu Historia ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu



**Jengo la Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar baada ya Mapinduzi hadi Mwaka 2014.**

**Vuga, Zanzibar.**

**NA HAMISA MMANGA - Wakili wa Serikali Mkuu.**

**AFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ina historia refu, iliyopitia kwenye awamu mbalimbali, kuanzia kipindi cha ukoloni hadi hapa tuliofikia.**

Hata hivyo katika vipindi vyote hivyo, Afisi hiyo imetekeleza vyema majukumu yake ipasavyo kulingana na mwelekeo awamu inayoongoza kwa wakati huo.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilirithiwa baada ya Mapinduzi na iliendelea kuwepo na kufanya kazi baada ya Mapinduzi lakini hakukuwa na Sheria mahsusi iliyoanzisha rasmi Afisi ya Mwanasheria Mkuu hadi mwaka 2013, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilipowasilisha Baraza la Wawakilishi Mswada wa Sheria na kupitisha Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu Nam. 6 ya 2013). Licha ya kuwa Mwanasheria Mkuu alikuwa akitambuliwa kupitia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na alikuwa akitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

# Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya Mapinduzi

Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni miongoni mwa ofisi kongwe hapa Zanzibar iliyoanzishwa mnamo mwaka 1914 wakati koloni la Kiingereza lilipoanzisha Baraza la Mahamia ya Kiingereza (Protectorate Council). Ushahidi wa hayo ni kwamba Mwanasheria Mkuu alikuwa ni mmoja wa wajumbe wa Baraza hilo.

Mwanasheria Mkuu kwa wakati huo alikuwa kiungo muhimu kama ilivyo sasa. Alikuwa ni mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria na Utawala (Legislative and Executive Council) la 1926. Baraza hili kazi yake kuu ilikuwa ni kutunga sheria na kumshauri Sultan katika masuala ya utawala. Aidha, Mwanasheria Mkuu aliendelea kufanya kazi zake hata katika Baraza la Kutunga Sheria na Utawala la mwaka 1936 na alikuwa ni miongoni mwa wajumbe wa Baraza hili lililodumu hadi Mapinduzi ya mwaka 1964. Katika kipindi cha ukoloni, Mwanasheria Mkuu mbali na kufanya kazi za kuishauri Serikali, alikuwa ana jukumu la kuandaa na kuchapisha sheria na kuandaa machapisho ya kisheria. Katika kazi kubwa aliyoifanya Mwanasheria Mkuu kwa wakati huo ni kuzikusanya na kuzijumuisha pamoja (Consolidation) Sheria za Zanzibar katika vipindi viwili tofauti. Majumuisho ya mwanzo yalifanyika mwaka 1926, na mwaka 1957 yalifanyika kwa mara ya pili. Majumuisho ya mwaka 1957 ni Sheria ambazo bado zinatumika ambazo zimewekwa pamoja katika vitabu vitano maarufu zinajulikana kama Vitabu Vyekundu (Red Books Volume I – Volume V).



***WOLFGANG DOURADO, Mwanasheria Mkuu wa Kwanza wa  Zanzibar Baada ya Mapinduzi.***

# Baada ya Mapinduzi kabla ya mwaka 2000

Mara tu baada ya Mapinduzi ya Mwaka 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alimteua Marehemu Wolfgang Dourado kuwa Mwanasheria Mkuu. Kwa wakati huo Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilikuwa katika Jumba la Wananchi Forodhani (People's Palace). Tofauti na kipindi cha Ukoloni, baada ya Mapinduzi Mwanasheria Mkuu hakuwa mjumbe wa Baraza la Mapinduzi wala Baraza la kutunga Sheria. Sheria ya "Legislatives Powers Decree" ya 1964 ambayo haikuwa na namba, ilitangaza kwamba mamlaka ya kutunga Sheria Zanzibar yatakuwa chini ya Baraza la Mapinduzi na ikawatangaza wajumbe Kumi na Nne wa Baraza hilo. Mwanasheria Mkuu hakuwa miongoni mwa wajumbe hao 14.

Mwanasheria Mkuu kwa wakati huo, aliendelea kufanya kazi zake za kuendesha mashtaka ya jinai tu pamoja na kuandaa miswada ya Sheria. Na haya yamethibitishwa na Katiba ya mwaka 1979 ambayo ilitambua uwepo wa Mwanasheria Mkuu katika Ibara ya 18 ya Katiba ambae atakuwa Mshauri Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Mwanasheria Mkuu katika Ibara ya 18(2) amepewa mamlaka ya kuendesha mashauri yote ya jinai kwa mujibu wa Sheria. Kwa kipindi hicho Mwanasheria Mkuu alijikita katika masuala ya jinai pekee na hakukuwa na mashauri ya madai licha ya kuwa Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8 Sheria za Zanzibar ilimtambua kuwa Wakili wa Serikali kwa mashauri yote ya madai ambayo yanaihusisha Serikali.



*Jengo liliowahi kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya Mapinduzi - People's Palace Forodhani.*

Baada ya Katiba ya mwaka 1979 kufutwa na kuundwa Katiba ya mwaka 1984, Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa Kifungu cha 56 alipewa jukumu la kuwa Mshauri Mkuu katika masuala ya Sheria na kuelezwa kuwa atafanya kazi nyengine atakazopangiwa na Rais. Katiba pia ilimtambua Mwanasheria Mkuu kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Baraza la Wawakilishi.

Kwa kuwa Katiba ya 1984 ilitambua haki za binaadamu na uhuru wa mtu binafsi, majukumu ya Afisi yalipanuka kwa uwepo wa utawala wa Sheria na Serikali ilianza kushtakiwa katika masuala ya madai hasa kuanzia kipindi cha miaka ya 1990. Hivyo Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilianza kupokea mashauri ya madai katika Mahakama Kuu ya Zanzibar.




***Jengo la Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuanzia 2014 hadi sasa - Mazizini Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.***

# Mwanasheria Mkuu na Afisi ya Kabidhi Wasii Mkuu

Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika kutekeleza majukumu yake, iliratibu kazi na majukumu yote ya Afisi ya Kabidhi Wasii Mkuu (Administrator General) (Administrator General) kuanzia mwaka 1974 hadi mwaka 1983.

Kwa wakati huo, Afisi ilisimamia masuala yote ya usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka, nyaraka, hati miliki, majina ya biashara, makampuni, pamoja na mambo mengine ya usajili ambayo kwa sasa yanaendelea kutekelezwa na Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara (BPRA) na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA)

Aidha, Afisi ya Mwanasheria iliendelea kutoa uthibitisho wa kutokuwa na pingamizi ya ndoa (Certificate of no impediment to marriage) kwa Wazanzibari walioko nje ya nchi waliotaka kufunga ndoa hadi mwaka 2015.



***Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya AG  wakiwa katika moja ya vikao vyao vya kazi.***

# Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuanzia mwaka 2000 hadi sasa

Afisi ya Mwanasheria katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 ilishuhudia mabadiliko makubwa na ilikuwa ikipiga hatua za maendeleo kila baada ya muongo mmoja. Katika kipindi cha miaka ya 2000 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilidhamiria kuimarisha Utawala wa Sheria na Utawala Bora. Aidha, utawala wa haki na sheria ulipewa kipaumbele

Baada ya mwaka 2000 Mwanasheria Mkuu alikuwa anaiwakilisha Serikali katika kesi za madai na jinai katika Mahakama ya Mkoa na Mahakama Kuu. Aidha, jeshi la polisi lilikuwa likifanya kazi mbili ya kupeleleza na kufungua mashtaka kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya. Kwa kipindi hicho Mwanasheria Mkuu ndiye aliyekuwa na uwezo wa kufungua mashtaka ya jinai na alikasimu mamlaka yake kwa Mawakili wa Serikali, jeshi la polisi na watu wengine aliyeona wanafaa kumuwakilisha.

Mabadiliko makubwa ya utawala bora na utawala wa sheria yaliyofanywa kipindi hicho yaliweza kupunguza mamlaka ya Mwanasheria Mkuu katika usimamizi wa kesi za jinai. Baraza la Wawakilishi lilipitisha Marekebisho ya Tisa ya Katiba ya 1984 na kuanzisha Afisi ya Mwendesha Mashtaka katika kifungu cha 56A. Lengo na madhumuni ya mabadiliko hayo ni kuimarisha utawala bora kwa kuanzisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambae atakuwa ndiye mwenye dhamana ya kuanzisha mashtaka ya jinai katika mahakama zote za Unguja na Pemba. Hatua hii ilimpa nafasi Mwanasheria Mkuu kujiimarisha zaidi katika kazi zake za ushauri na usimamizi wa kesi za madai pamoja na kuandaa miswada ya Sheria.

# Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Tume ya Kurekebisha Sheria

Tume ya Kurekebisha Sheria ilianzishwa kwa Sheria Nam. 16 ya mwaka 1986. Tume ilianza kufanya kazi ikiwa chini ya usimamizi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na ilitekeleza majukumu yake chini ya Afisi hiyo. Kwa kipindi hicho kabla ya 2013, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliweza kuajiri na kutekeleza majukumu mengine ya Tume. Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilifanikiwa kujenga Ofisi ndogo pembezoni mwa Jengo lililokuwa Wizara ya Katiba na Utawala Bora Vuga kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Tume ya Kurekebisha Sheria.

Kwa sasa Tume imekuwa ikiendelea na kutekeleza majukumu yake bila ya usimamizi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kuipunguzia majukumu kama ambavyo ilikuwa na majukumu katika usimamizi wa makosa ya jinai ambayo kwa sasa yapo chini ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.



***Baadhi ya Mawaikili wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakifuatilia  Kesi Mahakama Kuu (Tunguu).***

# Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Mawakili wa Serikali

Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Mawakili wa Serikali.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya 2013 ilikuwa na uhaba wa watendaji hasa mawakili wa Serikali. Kwa kipindi hicho Afisi ilikuwa na mawakili wa Serikali wasiozidi kumi ambao wakitekeleza majukumu yao ya kuishauri Serikali, kusimamia kesi za madai na kuandaa miswada ya sheria. Wakati huo wakili mmoja akifanya kazi zote kwa wakati mmoja  tofauti na ilivyo sasa wakili wa Serikali anajikita na eneo moja tu la kufanyia kazi ama kusimamia kesi za madai au kushauri katika masuala ya mikataba au kuandaa miswada ya sheria na hati nyengine za kisheria.

Aidha, mabadiliko makubwa yamefanywa ya kuimarisha utendaji na kuleta ufanisi katika kazi zake. Kwanza mawakili wa Serikali wameongezeka kutoka idadi ya mawakili Ishirini na Moja (21) ikijumuisha Mwanasheria Mkuu mwaka 2014 hadi Arobaini na Sita (46) mwaka 2023. La Pili ni kuweka mgawanyo wa majukumu kwa kuanzisha vitengo katika mwaka 2013 ambapo jumla ya vitengo vinne viliundwa ambavyo ni:

a. Kitengo cha Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai;
b. Kitengo cha Uandishi wa Sheria na Sera za Kisheria;
c. Kitengo cha Huduma za Ushauri na Usimamizi wa Mikataba; na
d. Kitengo cha Utawala.

Vitengo hivi vilisaidia kufanya kazi kwa uweledi na ufanisi na kumuwezesha wakili wa serikali kujikita katika eneo moja la kufanyia kazi. Hali hii pia imeimarishwa hadi 2018 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliporidhia muundo mpya na kuanzisha Idara Nne, Kati ya hizo, Idara Tatu ni za Sheria na moja ni ya Utawala. Aidha, vitengo vinne vilianzishwa katika muundo huo pamoja na Afisi ya Pemba. Muundo huo uliendelea kutumika hadi 2023 ulipofanyiwa marekebisho na kuendana na hali ya sasa. Kimuundo Afisi Mwanasheria Mkuu inaongozwa na Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Divisheni.



***Mawakili wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Afisi ya Pemba wakiwa katika picha ya pamoja.***

# Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba

Kwa miaka yote kabla ya 2020, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilikuwa na Afisi katika upande mmoja tu wa Zanzibar yaani Unguja na kwa upande wa Pemba ilikuwa ikitekeleza kazi zake pale inapoiwakilisha Serikali katika kesi ambazo zilifunguliwa katika Mahakama za Pemba. Kwa kipindi chote hicho Kamati za Baraza la Wawakilishi zilikuwa zikiwasilisha hoja ya kuwa imefika muda Afisi ya Mwanasheria Mkuu kufungua Afisi Pemba kwa ajili ya kuhudumia masuala ya kisheria kwa Afisi za Pemba. Aidha, ongezeko la kesi za madai za Serikali zinatoa hamasa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa na Afisi Pemba.

Kwa kuwa Muundo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ulitambua uwepo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba, uongozi haukuwa na sababu ya kukataa hoja ya Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi. Aidha, kufunguliwa Afisi ya Pemba kutapekelea kurahisisha usimamizi wa kesi za madai zilizofunguliwa Pemba na kuokoa gharama ya kupeleka wakili wa Serikali mara kwa mara kwa ajili ya usimamizi wa kesi husika. Mnamo Machi 2020, Afisi ilifungua rasmi Afisi zake hapo Gombani Chake Chake Pemba kwa ajili ya kutoa huduma za kisheria kwa upande wa Pemba. Afisi ina jumla ya Mawakili wa Serikali watatu (3) wanaofanyakazi za usimamizi wa kesi za madai na kutekeleza masuala mengine ya kisheria.

# Mwanasheria Mkuu apokea Rasimu za Sheria ya usuluhishi wa migogoro na uanzishwaji wa Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro



***Mwanasheria Mkuu katikati akipokea Rasimu ya uanzishwaji wa Sheria na Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro nje ya Mahkama kutoka kwa Mshauri Elekezi, Dkt. Alex Nguluma wa Kampuni ya Rex Attorneys ya Dar es Salaam, kushoto ni Naibu Mwanasheria Mkuu Shaaban Ramadhan Abdalla.***

***Na Mwandishi wetu***

***MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji, amesema uanzishwaji wa Sheria na Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro nje ya Mahkama (ADRC), kutapelekea muelekeo mzuri zaidi wa sekta ya uwekezaji***

Dkt. Mwinyi ameyasema hayo mara baada ya kupokea rasimu ya Sheria ya Usuluhishi wa Migogoro pamoja na Rasimu ya Sheria ya Uanzishaji wa Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro kutoka kwa Mshauri Elekezi, Dkt. Alex Nguluma wa Kampuni ya Rex Attorneys ya Dar es Salaam, katika hafla iliyofanyika Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Mazizini.

Alisema kuwepo kwa Sheria na kituo hicho Zanzibar ni jambo la lazima kutokana na



***Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji, akizungumza machache mara baada ya kupokea rasimu ya uanzishwaji wa Sheria na Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro nje ya Mahkama.***

kasi ya uwekezaji unaondelea kufanyika nchini, sambamba na wawekezaji kuongeza imani kuweka miradi yao Zanzibar.

Alisema kituo hicho pia kunaakisi mtazamo wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, katika dhamira yake ya kuimarisha na kurahisisha mazingira ya uwekezaji ili kukuza maendeleo nchini.

Mwanasheria Mkuu huyo alisema kituo hicho kitasaidia suluhu na maridhiano pale migogoro ya kibiashara na uwekezaji inapotokea na hivyo kuibakisha sekta ya uwekezaji nchini katika hali ya utulivu.

Aliwashukuru washauri elekezi kwa namna walivyojitahidi kufanya utafiti wa kina ili kuhakikisha kuwa wanakuja na Sheria muhimu ambayo inakidhi mahitaji ya Zanzibar.

Kwa upande wake Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban Ramadhan Abdalla, alisema kukamilika kwa Kituo hicho kutasaidia kutatuliwa kwa migogoro kwa haraka, na kinatarajiwa kuchochea zaidi ongezeko la Wawekezaji wanaokuja Zanzibar kwa vile Wawekezaji hao watakuwa na amani na uwekezaji wao nchini.

Naibu Shaaban alisema Sheria iliyopo ya Utatuzi wa Migogoro Sura Nam. 25 ya mwaka 1928 imepitwa na wakati kwa vile ilianzishwa enzi za ukoloni na haiendani na kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia ambayo yamefikiwa nchini.

Alibainisha kuwa kulingana na kasi ya ukuaji wa uchumi, teknolojia na shughuli mbali mbali za kiuwekezaji Sheria hiyo inahitaji kuimarishwa zaidi ili kwenda sambamba na kasi ya maendeleo.

"Mambo yatakapokamilika tutaifuta 'Arbitration decree' na tutakuja na 'Arbitration Act' pamoja na kanuni ambazo zitasaidia kutatua migogoro kwa wakati tulionao", alifafanua Naibu Mwanasheria Mkuu.

Alifahamisha kuwa, katika hali ya kawaida migogoro inapotokea hupelekwa mahkamani lakini kuna baadhi ya migogoro haihitaji kuwa na taratibu nyingi na za muda mrefu kutatuliwa kwake.

Kwa upande wake, Mrajisi wa Mahkama Kuu Zanzibar,



***Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar Shaaban R. Abdalla akifungua kikao cha kupokea maoni kuhusu Rasimu za Sheria ya usuluhishi wa migogoro na uanzishwaji wa Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro.***

Valentina Andrew Katema, alisema kuanzishwa kwa kituo cha utatuzi wa Migogoro nje ya Mahkama ADR Center kutasaidia kutatua migogoro kwa haraka na kuipunguzia mzigo Idara ya Mahkama.

Alieleza kuwa, utaratibu wa kwenda Mahkamani ni kwenda kupata hukumu ya kushinda kesi au kushindwa jambo ambalo wakati mwingine haliachi picha nzuri miongoni mwa walioshitakiana mahkamani.

Mrajis huyo alisema watu watakapoamua kwenda kutatua mgogoro wao katika Kituo kuna uwezekano mkubwa wa kubakia katika mahusiano mema kwa vile hakuna kushindwa wala kushinda bali ni kufikia makubaliano ya pande zilizokuwa na mgogoro.

Akizungumzia faida za Kituo hicho, Bi. Valentine alisema kuwepo kwa ADR Center kutachochea shughuli na fursa nyingi za kimaendeleo kwa vile Wawekezaji watakuja kwa wingi wakijua kwamba kuna namna nzuri ya kusuluhisha Migogoro pale inapoibuka.

"Wenzetu wawekezaji wanapokuja kitu cha msingi huzingatia sana usalama wa uwekezaji wao na hawapendi kupelekwa mahkamani kutokana na gharama za Mahkama na kuchukuwa muda mrefu, lakini ADRC itawarahisishia kwa vile kunapotokea shida watafika hapo kwa ajili ya kutatua tatizo nje ya Mahkama",alifafanua.

Kwa upande wake mmoja wa Washauri elekezi Dkt. Fauz Twaib, ambaye ni Jaji Mstaafu na Rais wa Jumuiya cha Wanasheria Afrika Mashariki amesema lengo la kazi wanayoifanya ni kuleta Sheria ambayo itaweka masharti ya jinsi gani Sheria za usuluhishi hasa wa migogoro zinavyotakiwa kufanyakazi Zanzibar kwa zama za sasa.

Alisema kupitia kazi hiyo wanakusudia kuubadilisha mfumo wa Sheria hizo za utatuzi wa migogoro ambao kwa sasa sheria yake ina zaidi ya miaka 100 toka kuanzishwa kwake na kwamba haiendani tena na hali halisi.

Dkt. Fauz amefahamisha kuwa kazi yao kubwa ni kuandaa sheria mbali mbali hasa Sheria hiyo ya usuluhishi lakini pia wamependekeza kituo maalum kwa ajili ya utatuzi wa Migogoro ingawa haitoshughulika na maswala yote kwa vile migogoro mengine itapelekwa katika Mahkama za kawaida.

Naye Mshauri Elekezi, Dkt. Alex Nguluma ameshukuru Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa kuiamini Taasisi yao na kuahidi ushirikiano ili kuhakikisha lengo la Serikali la kutaka kuanzisha Sheria na Kituo cha usuluhishi wa migo-goro linatimia.

Alisema sheria hizo zinalenga kuboresha utatuzi wa migogoro hasa kwa jamii ya wawekezaji na wafanyabiashara ili kuhakikisha Zanzibar inakuwa kituo kikubwa na salama kwa uwekezaji.

Aidha Dkt. Nguluma alisema kuwa, katika sheria hiyo wamejitahidi kuandaa sheria ambazo zitasaidia kuepukana na matatizo ya rushwa kwa kuwabana Wanasheria na Majaji ambao watashiriki moja kwa moja katika Kituo hicho ili kila mwenye haki apate haki yake.

# MATUKIO KA




*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji akizungumza katika kilele cha siku ya Sheria huko Viwanja vya Mahkama kuu Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja.*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwiny Wadau uliojadili Rasimu za Miswada ya Sheria Usuluhishi wa Migogoro Zanzibar, huko Golde*



*Mwanafunzi Nahla Mohammed wa Skuli ya Fuoni akiuliza maswali wakati Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilipofanya Mkutano na Wananchi wa Shehia ya Fuoni kwa lengo la kutoa elimu ya kisheria kuhusu mambo mbali mbali.*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwin pamoja na Kamati ya Kutathmini Ufanisi n Ushirikiano wa Afrika Mashariki huko Afisini*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji akizungumza katika Kikao na Kamati ya kudumu ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi iliyofanya ziara katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini.*



*Mwanasheria Mkuu Zanzibar Dkt. Mwinyi Ta na baadhi ya Wafanyakazi wa Afisi yake mar Abdalla (kulia waliokaa) ambaye amestaafu*

# ATIKA PICHA



*yi Talib Haji akizungumza katika Mkutano wa ya Usuluhishi na Sheria ya Kuanzisha Kituo cha n Tulip Uwanja wa Ndege Zanzibar*



*Mwanasheria Mkuu Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji kulia akibadilishana mawazo na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mh. Hemed Suleiman Abdulla katika halfa ya kuwasilishwa kwa Ripoti ya CAG Viwanja vya Ikulu mjini Zanzibar.*



*yi Talib Haji (katikati) akiwa katika picha ya a Utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na kwake Mazizini, Zanzibar.*



*Wakili Mwandamizi Ali Ali kushoto akibadilishana mawazo na Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar mara baada ya kusikiliza Kesi ya Mahkama ya Rufaa huko Mahkama kuu Tunguu Kusini Unguja*



*lib Haji (katikati) akiwa katika Picha ya pamoja a baada ya hafla ya kumuaga Bi Masunya Juma katika Afisi hiyo.*



*Mawakili wa Serikali wakikagua eneo lenye mgogoro huko Pwani Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja*

# Ufahamu mchakato wa kutunga Sheria




## MCHAKATO WA KUTUNGA SHERIA ZANZIBAR

***Na Salim M. Abdalla - Wakili wa Serikali Mwandamizi, Afisi ya Mwanasheria Mkuu***

***Kwa mujibu wa kifungu cha 78 (1) cha Katiba ya Zanzibar, 1984 Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ndicho chombo kilichopewa uwezo wa kutunga sheria Zanzibar.***

Baraza la Wawakilishi lina mamlaka ya kutunga sheria kwa mambo yote yasiokuwa ya Muungano yanayohusu Zanzibar. Hata hivyo, zipo taratibu na hatua mbali mbali za awali kabla ya Mswaada wa sheria kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutungwa kuwa sheria.

Kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) (f) cha Sheria ya Kuanzishwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nam. 6 ya 2013. Afisi ya Mwanasheria Mkuu imepewa jukumu la kutayarisha Miswada ya Sheria au kusababisha mapendekezo ya sheria kutayarishwa na kuwasilishwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mapinduzi kwa mapitio.

Miswada inayowasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi inaweza kugawanywa katika aina tatu kuu kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

1. Mswada wa Serikali: Huu ni Mswada unaowasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
2. Mswada wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi: Mswada huu unawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi na Mwenyekiti au Mjumbe yeyote wa Kamati ya Kudumu kwa niaba ya Kamati hiyo.
3. Mswada wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi: Mswada unawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi na mjumbe ambaye si Waziri wala Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mswada wa Serikali huanza kama wazo linalotokana na idara au taasisi ndani ya Wizara. Kwa kawaida, wazo la kupendekeza kutungwa kwa Sheria Mama hutokana na vyanzo mbalimbali kulingana na aina ya changamoto za kisheria au tatizo ambalo Wizara au Taasisi inakabiliana nalo.

Wazo la kutunga sheria linaweza kutokana na Serikali kupitia Wizara au Taasisi zake, uamuzi wa Mahakama, sekta binafsi, jumuiya za kiraia au mwanajamii. Mswada unaweza kutayarishwa mwanzoni na watu

au vikundi vyenye maslahi ya aina moja. Wazo hilo huchukuliwa na kuzingatiwa na taasisi husika ndani ya Wizara ambapo huandaliwa na kuwa Rasimu ya Mswada wa Sheria.

Baadhi ya Miswada inaweza kuandikwa na wafanyakazi wa Wizara kwa ombi la Mamlaka husika na baadhi inaweza kuandikwa na wanasheria waliojiriwa na watu au taasisi zenye maslahi na sheria husika. Hata hivyo, ushiriki wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni muhimu katika hatua za awali ili kudhibiti ubora na kuhakikisha kuwa Mswada unakidhi viwango vya uandishi wa sheria. Ikumbukwe kwamba, ushiriki wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni matakwa ya kisheria (Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa (Utekelezaji wa Majukumu), Namba 6 ya Mwaka 2013).

Kwa madhumuni ya kuliendeleza wazo kuwa Rasimu ya Mswada, idara au taasisi husika inatakiwa kuunda timu ya wataalamu inayojumuisha Afisa kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ili kusaidia masuala ya kiuandishi na kisheria katika mchakato wa utayarishaji wa Rasimu ya Mswada.

Timu inapomaliza kuandaa rasimu ya awali ya mswada, Wizara au taasisi husika kwa kushirikiana na timu iliyoaandaa rasim hiyo, huipeleka rasimu hiyo kwa wadau ili kupata maoni yatakayosaidia kuuweka vyema.

Baada ya timu kujumuisha maoni kutoka kwa wadau, rasimu ya mwisho itawasilishwa kwenye manejimenti ya idara au taasisi husika na hatimaye kupelekwa kwa Kamati Tendaji ya Wizara na Kamati ya Uongozi ya Wizara, kwa ajili ya kujadiliwa na kuzingatiwa.

Taratibu zote zinazohitajika zikikamilika, Wizara itawasilisha Waraka kwa Kamati ya Makatibu Wakuu kwa hatua za kujadiliwa na kupata kibali cha kuiwasilisha Baraza la Mapinduzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 39(6)(a) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Na. 2 ya 2011, Kamati ya Makatibu Wakuu ni chombo cha kitaalamu ambacho kina wajibu wa kupitia pendekezo lolote linalohusu Mswada wa Sheria, kabla ya kuwasilishwa Baraza la Mapinduzi.

Hivyo, Waraka wa Baraza la Mawaziri pamoja na Mswada unaopendekezwa utawaasilishwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu na Katibu Mkuu wa Wizara husika au Naibu Mwanasheria Mkuu kwa jambo linalohusu Afisi ya Mwanasheria




***Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji, akichangia katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi huko Chukwani Zanzibar.***




***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi akisaini Sheria mpya mwaka 2024 katika viwanja vya Ikulu Zanzibar.***

Mkuu, kwa lengo la kujadiliwa, kuzingatiwa na kuamuliwa.

Baada ya Kamati ya Makatibu Wakuu kumaliza hatua za kujadili na kuzingatia Waraka pamoja na Rasimu ya Mswada unaohusika, Waziri au Mwanasheria Mkuu kwa Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali, atawasilisha Baraza la Mapinduzi Waraka pamoja na Rasimu husika.

Katibu Mkuu Kiongozi atawasilisha maoni ya Kamati ya Makatibu Wakuu kuhusiana na Rasimu ya Mswada. Baraza la Mapinduzi litaujadili Waraka unaoombewa kibali cha kuidhinisha utungwaji wa sheria na kutoa maamuzi. Iwapo kibali kitatolewa, Waziri husika na Mwanasheria Mkuu watapewa maagizo ya kuweka vizuri pendekezo lililokubaliwa katika rasimu ya Mswada.

Endapo, Baraza la Mapinduzi litaridhia, Rasimu ya Mswada itawasilishwa kwenye Kamati ya Masuala ya Katiba na Sheria ya Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya mapitio, uchunguzi na maoni. Baada majadiliano hayo, Kamati itatoa taarifa kwa Baraza la Mapinduzi, kwa ajili ya kuidhinishwa.

Katibu Mkuu Kiongozi atawasilisha Azimio la Baraza la Mapinduzi kwa Mwanasheria Mkuu na kueleza mapendekezo kuhusu mambo mapya ya kujumuishwa na kuwa sehemu ya Rasimu ya Mswada au mambo ya kutolewa ambayo hayatakiwi kuwa sehemu ya Mswada huo.

Agizo la kuandaa Mswada wa Sheria kwa kawaida hutokana na taarifa za kisera, mapendekezo ya ripoti za utafiti, maswali au maamuzi ya mahakama. Mara baada ya kibali cha Baraza la Mapinduzi kutolewa, maelekezo ya kuandaa rasimu yanaweza kutolewa kwa Mwanasheria Mkuu.

Mwanasheria Mkuu baada ya kupokea maelekezo kutoka Baraza la Mapinduzi atatayarisha Mswada wa Sheria kwa kuzingatia kile kilichoidhinishwa na Baraza la Mapinduzi.

Mwanasheria Mkuu anaweza, anapoona inafaa, kushirikiana na Wizara inayohusika au taasisi zinazohusiana na mswada huo.

Baada ya Mwandishi wa Sheria kupata kibali cha kuandaa Mswada kwa ajili ya kupelekwa Baraza la Wawakilishi, Mswada huo huandaliwa na Waziri anayehusika kusaini. Baada ya hatua hiyo, Mswada utachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kwa maagizo ya

Mwanasheria Mkuu.

Kuchapishwa kwa Mswada katika Gazeti Rasmi ni matakwa ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Kanuni hizo zinaeleza kuwa Tangazo la Kwanza la Mswada wa Sheria litafanyika katika Gazeti Rasmi la Serikali ndani ya siku ishirini na moja, kabla ya Mswada ya kuwasilishwa kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo, Masharti haya hayatumiki kwa Mswada unaowasilishwa Baraza la Wawakili kwa hati ya dharura (Rejea Kanuni ya 83(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

Baada ya Mswada huo kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, Mwanasheria Mkuu atauwasilisha Mswada huo kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa hatua zinazofuata za kutunga sheria, kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Kudumu za Baraza. Kimsingi, Mswada hupitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kusomwa mara tatu.

Mswada utasomwa kwa Mara ya Kwanza wakati unawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika au Mwanasheria Mkuu, kama itakavyokuwa, ambapo husomwa jina refu (long title) la Mswada.

Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, kabla ya Mswada kuwasilishwa kwenye kikao cha Baraza, kila mjumbe wa Baraza hupewa nakala ya Mswada huo kwa maandalizi. Katika maandalizi hayo kila mjumbe anatakiwa kuitisha kikao katika eneo lake la uchaguzi ili kukusanya maoni ya wananchi juu ya Mswada huo.

Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayohusika na Mswada itapewa Msawada na Kamati kujadili Mswada huo na kupendekeza marekebisho ambayo huwasilishwa katika Kikao cha Baraza.

Katika kuupitia Mswada huo, Kamati inaweza kualika wadau kwa ajili ya kupata maoni kuchangia Mswada huo. Wadau hao wanaweza kutoa maoni ambayo Kamati inaweza kukubaliana nayo au kuyakataa.

Hatua ya Mswada kusomwa kwa Mara ya Pili hufanyika kwa Waziri anayehusika na mswada huo au Mwanasheria Mkuu




***Zaituni Simba, Mwanasheria kutoka AGC akiwa katika Mchakato wa Uandishi wa Sheria.***

kutoa taarifa fupi ya Mswada na kufuatiwa na Taarifa ya Kamati iliyojadili Mswada huo.

Kwa kawaida, Mwenyekiti wa Kamati huwasilisha Taarifa ya Kamati. Baada ya Hotuba ya Kamati, wajumbe hupewa nafasi ya kuchangia Mswada huo, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Baada ya Wajumbe kuchangia, Waziri anayehusika hupewa fursa ya kufanya majumuisho na kutoa hoja. Endapo hoja itakubaliwa, Waziri ataliomba Baraza kukaa Kamati ya Kutunga Sheria, kwa ajili ya kupitisha Msawada kifungu kwa kifungu.

Mswada Kusomwa kwa Mara ya Tatu ni hatua ya mwisho katika hatua za Baraza la Wawakilishi kupitisha Mswada. Hatua hiyo hufanyika baada ya Kamati ya Kutunga Sheria kukamilisha kazi ya kupitisha vifungu vya Mswada na Waziri au Mjumbe anayehusika kuliomba Baraza Mswada usomwe kwa Mara ya Tatu.

Hoja hiyo ikikubaliwa, Katibu wa Baraza au mwakilishi wake atasoma jina la Mswada kwa ukamilifu wake (Long Title) na Mswada kupitishwa rasmi.

Baada ya Baraza kukamilisha kazi yake, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwa kushiriakiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu huatayarisha nakala ya mwisho ya Mswada na Katibu hutia saini nakala hiyo na kuiwasilisha kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye akiafiki Mswada huo, atautia saini na kuwa Sheria, kwa masharti ya Katiba ya Zanzibar, 1984.

Rais baada ya kutia saini Mswada uliopitishwa na Baraza la Wawakilishi, Mswada huo utachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na kutangazwa kutumika kwake.

Kwa ufupi, Utungaji wa Sheria ni utaratibu unaopitia hatua mbalimbali ili kukidhi haja ya kuwepo Sheria inayotosheleza mahitaji kwa wakati inapohitaka. Mswada unaweza kutayarishwa kutoka katika chanzo chochote kati ya Serikali kupitia Wizara, Sekta Binafsi, Baraza la Wawakilishi, Jumuiya za Kiraia au jamii.

Hatimaye, Mswada hufikishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa hatua zaidi na Baraza la Mapinduzi (kama ni Mswada wa Serikali). Mwisho, Mswada hufikishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa Utungwaji wa Sheria, kwa kuzingatia Katiba ya nchi, Sheria na Kanuni zinazohusika na Utungaji wa Sheria na baadaye huchapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali kwa ajili ya kurasmisha matumizi yake.



# Afisi ya Mwanasheria Mkuu, wadau wajadili Rasimu mapitio ya sheria



***Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban Ramadhan Abdalla, akifungua kikao cha wadau kupitia Rasimu ya Mswaada wa Mapitio ya Sheria kilichofanyika katika Afisi hiyo Mazizini Zanzibar.***

***Na Mwandishi wetu***

***AFISI ya Mwanasheria Mkuu, inakusudia kuzifanyia mapitio sheria zote za Zanzibar ili kuzikusanya na kuziweka pamoja kwa lengo la kusaidia urahisi wa kuzisoma sheria hizo***

Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban Ramadhan Abdalla, ameyasema hayo wakati akifungua kikao cha wadau kupitia rasimu ya mswaada wa Mapitio ya Sheria kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Afisi hiyo Mazizini Zanzibar.

Alisema zoezi la kuzifanyia mapitio sheria za Zanzibar zitajumuisha pia na sheria zote zinazotumika kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Katika kufanikisha kazi hiyo, Naibu Shaaban alisema Afisi imeandaa mswaada wa kuifuta Sheria ya Mapitio ya mwaka 1961 na kuiandika upya sheria hiyo.

Alibainisha kuwa kukamilika kwa hatua hiyo ya marekebisho ni moja katika ya hatua muhimu ambazo Afisi yake imekuwa ikizichukua katika kuimarisha sekta ya Sheria Zanzibar.

Naibu Shaaban alisema ipo haja ya kuzikusanya pamoja kwa kuzipitia Sheria zote za Zanzibar na kuziweka katika Vitabu vya Sheria (Statute books) ili kurahisisha upatikanaji na usomaji wa sheria hizo kwa mtu yeyote anayehitaji.

Alifahamisha kuwa katika kufikia hatua hiyo, kunahitajika kupatikana muongozo ambao ndiyo Sheria ya Mapitio ya Sheria

inayotoa nguvu kwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kuchukua hatua mbali mbali kufikia lengo hilo.

Hivyo, alitumia fursa hiyo kuwaomba wadau watakaoshiriki kutoa maoni katika rasimu ya mswaada huo, kuwa huru katika kuwasilisha maoni yao ili kusaidia kupatikana sheria bora itakayorahisisha upatikanaji wa Sheria zote kwa urahisi.

Akielezea hatua za kupatikana Sheria hiyo, Naibu Mwanasheria Mkuu amefahamisha kuwa, mara baada ya Wadau kutoa maoni yao mswaada huo utawasilishwa na kujadiliwa katika kikao cha Kamati ya ongozi ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, baada ya hapo, Mswaada huo utajadiliwa katika kamati ya kitaalam ya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Baada ya hapo hatua itakayofuata ni kuwasilishwa katika Baraza la Mapinduzi (BLM) ili kuiridhia na mwisho kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa kujadiliwa.

"Madhumuni yetu makubwa ni kuhakikisha ndani ya mwaka huu katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kijacho mwezi wa Septemba angalau Mswaada huo utajwe kwa mara ya kwanza katika Baraza hilo" Alisema Naibu Mwanasheria Mkuu.

Akiwasilisha mswada huo kwa Wadau, Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uandishi wa Sheria, Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Salim M. Abdalla alisema kwa muda mrefu umekuwa utamaduni wa sheria inapohitajika kufanyiwa marekebisho, hufanyika marekebisho.

Alisema baadhi ya sheria hufutwa hali inayowapelekea wananchi na wadau wa sekta sheria kupata tabu ya kuzipata sheria hizo na kuzisoma kwa pamoja na marekebisho yake.

Wakili huyo alisema Afisi ya Mwanasheria mkuu inakusudia kuziweka pamoja sheria mama pamoja na sheria ndogo ili kurahisisha kusomeka kwa pamoja na marekebisho yake.

Kuhusu sheria iliyopo sasa Wakili Salim alisema, imepitwa na wakati kutokana na kupitishwa kwake tangu mwaka 1961, hivyo haiendani na hali halisi ya mapitio ya sheria katika zama za sasa.

"Kimsingi sheria iliyopo haiwezi kukidhi haja wala haiwezi kutusaidia kupata sheria bora ya mapitio ya sheria", alisema Wakili Salim.

Miongoni mwa Wadau wa Sekta ya Sheria walioshiriki kutoa maoni katika mswaada huo ni pamoja na Mahkama Kuu, Tume ya kurekebisha Sheria, Skuli ya Sheria Zanzibar, Baraza la wawakilishi na Mawakili wa serikali wanaofanya kazi katika Wizara na taasisi mbali mbali za Zanzibar.



***Wakili wa Serikali Mwandamizi, Salim M. Abdalla akiwasilisha Rasimu ya Mswaada wa Mapitio ya Sheria kwa wadau katika ukumbi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini, Zanzibar.***

# Mwanasheria Mkuu asihi nidhamu kwa watendaji



***Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar (AG), Dkt. Mwinyi Talib Haji, akimkabidhi Cheti Mfanyakazi mstaafu wa Afisi hiyo Bi. Masunya Juma Abdalla katika hafla iliyofanyika AGC.***

***Na Mwandishi wetu***

**MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar (AG), Dkt. Mwinyi Talib Haji, amewataka watendaji wa taasisi hiyo, kuiga tabia njema za wafanyakazi wastaafu ikiwemo utunzaji siri za ofisi ili kujiweka salama wao na ofisi wanazozifanyia kazi.**

Dkt. Mwinyi alitoa wito huo katika hafla ya kumuaga aliyekuwa katibu Muhtasi wa Afisi hiyo ambaye amestaafu Bi. Masunya Juma Abdalla, huko katika ukumbi wa Afisi hiyo Mazizini Mjini Unguja.

Alisema ni jukumu la kila mtendaji kuiga na kutekeleza mwenendo mwema aliokuwa nao Bi. Masunya ikiwemo kufanya kazi kwa bidii, nidhamu na ustahamilivu. Dkt. Mwinyi alisema Bi Masunya alitanguliza uzalendo na maslahi ya nchi kwa kuamini kuwa Taasisi anayofanyia kazi ni muhimu ambayo inahitaji mtu mwenye bidii ya kazi jambo lililomjengea sifa ya kuwahi kazini na kuchelewa kutoka siku zote.

Aliwataka wafanyakazi hao kila mmoja kuweka nia na mikakati ya kuhakikisha anaagwa kwa wema kutokana na utumishi wake uliotukuka kama ilivyofanyika kwa Bi Masunya. "Kukusanyika hapa tukafurahia kumuaga mwenzetu ni kwa sababu ya wema wake na utendaji wake uliotukuka, angekuwa Mtu muovu hapa tusingekuwepo hivyo kila mmoja wetu afikirie namna ya kutenda wema zaidi", alisema Mwanasheria Mkuu.

Alimtaka mstaafu huyo kuendelea kutembelea ofisini kila anapopata muda na kutoa ushauri ambao anaona unafaa katika kupeleka gurudumu la maendeleo mbele.

Kadhalika Dkt. Mwinyi aliwataka wafanyakazi wa Afisi hiyo nao kuendelea kumkumbuka na kumtembelea ili kuzidi kuimarisha udugu na uhusiano mwema ambao aliuacha ofisini.

Mwanasheria Mkuu huyo aliwakumbusha wafanyakazi kuzidisha mapenzi miongoni mwao hasa kwa kuzingatia kuwa maeneo ya kazi ndio sehemu ambayo mtumishi wa umma hutumia muda mwingi, hivyo ni muhimu kuwa wastahamilivu na moyo wa kusameheana wao kwa wao.



***Wafanyakazi wa Afisi ya AG katika picha ya pamoja katika hafla ya Kumuaga Bi. Masunya Abdalla.***

"Kazini ndio sehemu mnayokutana na kutumia muda mwingi sasa, bila kuwa na utaratibu wa kusameheana na kuvumiliana itakuwa ni chanzo cha kugombana na kusababisha matatizo na mwisho kuharibu kazi", alinasihi Dkt. Mwinyi.

Kwa upande wake, Naibu Mwanasheria Mkuu, Shaaban Ramadhan Abdalla alisema Bi. Masunya aliheshimu na kufuata vyema misingi na maadili ya utumishi wa umma kwa kufanya kazi kwa bidii na nidhamu ya hali ya juu kazini.

"Kwa kweli licha ya umri wake kuwa mkubwa, lakini Bi. Masunya alikuwa mpole na nidhamu ya hali ya juu, alikuwa anawahi kazini na kuondoka baada ya muda wa kazi, na ilikuwa jambo la nadra sana kuomba udhuru", alimsifia Naibu Mwanasheria Mkuu. Akitoa neno la shukran Bi. Masunya aliishukuru Afisi hiyo kwa wema wake hasa viongozi kutokana na moyo wa upendo waliomuonesha kipindi chote cha utendaji kazi wake.

Alisema miaka yote 41 aliyofanyakazi alipata mashirikiano mema huku akitoa mfano wa namna mwanawe aliyekuwa mgonjwa Afisi hiyo ilishirikiana naye kikamilifu katika matibabu na kumfariji kwa muda wote. "Katika kipindi kigumu cha kumuuguza mwanangu ambaye kwa sasa ni Marehemu nilipata kila aina ya ushirikiano, sikupewa maneno makali kwa kukosa kazini baadhi ya siku na kila Mfanyakazi alisimama na mimi katika kunifariji hadi pale mwisho wa uhai wa Mgonjwa", alisimulia Bi. Masunya.

Hivyo aliwasisitiza wafanyakazi hao licha ya kufanyakazi kwa bidii wajiwekee mazoea ya kuzidisha kutoa sadaka kwa wahitaji wakiwemo wangonjwa na wajane pale wanaponafasika kwani sadaka huimarisha upendo na kuondosha mabalaa. Katika hafla hiyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilimzawadia mstaafu huyo vitu tofauti ikiwemo, mabati, mifuko ya saruji na zulia.

# Kibonzo..



NAMUACHIA MUNGU, KIWANJA CHANGU KIMEGHUKULIWA HALAFU NAHANGAISHWA MIAKA YOTE...
UTAHANGAIKA SANA, WATOA MSAADA WA KISHERIA WAPO LAKINI HAMUWATUMII.
2023.

# Nasaha

## SHAIRI NA SALUM VUAI ISSA (*AFISI YA M*

1
Ilahi nipe nafasi, Shairi kulitongoa,
Ninene kadamnasi, Umuhimu wa Sheria,
Pasi shaka na kisisi, Elimu nipate toa,
Nitambulishe Ofisi, Ya Mwanasheria Mkuu.

2
Ni sawasawa na mfu, Nchi isiyo Sheria,
Matendo mengi machafu, Waovu tajitendea,
Mchana bila ya khofu, Siwepo wa kukemea,
Ofisi hii muhimu, Penye utawala bora.

3
Ofisi Meanza mbali, Kabla ya kujikomboa
Kushauri Serikali, Kuonesha njema njia,
Itekeleze shughuli, Kunufaisha raia
Mwanasheria Mkuu, Ofisi imetimia

4
Idara zake ni hizi, Ni nne nawatajia
Kwanza ya usimamizi, Kesi inazopokea
Na kuyafanyia kazi, Mashauri ya madai pia
Twashukuru Serikali, Ofisi kutuundia

5
Nyengineyo ni Idara, Uandishi wa Sheria
Ambayo pia kinara, Wa sera za kisheria
Utendaji wake bora, Serikali meridhia
Twajivunia Ofisi, Mwanasheria Mkuu

6
Na Idara ya huduma, Na ushauri kutoa
Hii imebeba dhima, Mikataba kupitia
Kikanda haiko nyuma, Na kimataifa pia
Jukumu ililopewa, haya kuyasimamia

7
Ili lisimame jengo, Msingi hutegemea
Hivyo Idara Mipango, Haikusahauliwa
Kuyatimiza malengo, Isiwe kusuasua
Na Rasilimali Watu, Ndio moyo wa ofisi

# a za Mshairi

## MWANASHERIA MKUU DIRA YA MAENDELEO)

**8**

Ofisi imeanzishwa,
Na kisha ikapitishwa,
Huduma merahisishwa,
Yano majukumu yake,

Kwa namba sita Sheria
2013 Miladia
Sote twazifurahia
Kwa utuo nawambia

**9**

Kuwakilisha Hukuma,
Na taasisi za umma,
Inajiendesha vyema,
Aidha hutayarisha,

Inapopata kadhia
Zote inasaidia
Madai kitokezea
Mashauri ya madai

**10**

Huandaa Miswaada
Ili kuondoa shida,
Inafanya jitihada,
Ina majukumu mengi,

Na hati za kisheria
Mambo yende kwa murua
Penye haki kutetea
Mengine nawawekea

**11**

Kabla kufunga kitabu,
Dokta Mwinyi Talibu,
Kamanda mtaratibu,
Pamwe na wake Naibu,

Na kalamu kuachia
Namvulia kofia
Ameshika makasia
Shaaban Ramadhani

**12**

Hao ndio viongozi,
Vijana wapiga kazi,
Pia na wafanyakazi,
Wote ni kitu kimoja,

Timamu wamebobea
Tunawatumainia
Wote bila kubagua
Wamesafi zao nia

**13**

Maadili ndio ngao,
Wote kwa umoja wao,
La leo hutendwa leo,
Anaekwenda na haja,

Wanayoishikilia
Ofisi wainyanyua
Sio kesho kungojea
Hutoka ameridhika

**14**

Hapa naweka kituo,
Wapate mafanikio,
Wang'are kila uchao,
Nasi tu pamoja nao,

Kwa Mola kuwaombea
Rabbi takabali dua
Nchi kuitumikia
Bega kwa bega sawia

# KIKOSI CHA AFISI YA MWANASHERIA MKUU




AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

**Fuatilia kurasa zetu za mitandaoya kijamii.**

**Afisi_ya_mwanasheriamkuu_znz**

SCAN ME